# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI KWENYE MKUTANO MKUU WA 12 MWAKA WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA MAJITAKA MIJINI TAREHE 27 APRILI 2010 MJINI MUSOMA

**1. Utangulizi:**

Natanguliza shukrani zetu kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema na Amani aliyetuwezesha kufikia siku ya leo na kukutana hapa Mjini Musoma. Kwa niaba ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, na kwa niaba yangu Mwenyewe, nachukua fursa hii kuwashukuru wote mlioitikia wito wa kuja kushiriki katika mkutano huu muhimu. Nikiwa Waziri mwenye dhamana katika sekta hii ya maji nawakaribisha washiriki wote wa mkutano huu. Nashukuru kwa mara nyingine tena kupata fursa ya kushiriki Mkutano huu kwa mara ya pili tangu niteuliwe kuwa Waziri mwenye dhamana katika sekta ya maji. Kwetu sisi wanasiasa, ambao ajira zetu hazina kipengele cha muda, fursa kama hii ni adimu na inapaswa kuenziwa.

**Ndugu Wajumbe**, huu ni mkutano wa kumi na mbili wa mwaka wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini, tangu Mamlaka hizi zianzishwe mwaka 1998. Lengo kubwa la Mkutano wa Mwaka huu, ni kujadili changamoto zinazozikabili Mamlaka hizi katika uendeshaji na utoaji wa huduma ya maji safi na uondoaji wa majitaka kwenye miji husika. Tunatakiwa kutathmini mikakati ya kuboresha huduma katika kutimiza malengo ya MKUKUTA, Milenia na Dira ya Taifa ya kuondoa umaskini na kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi karibu kabisa na makazi yao. Tathimini ya mikakati ni katika uendelezaji wake. Mikakati yote hii ambayo ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002. Sera inaelekeza kuwa maji yanayosambazwa lazima yawafikie wananchi wanaoishi mijini, pembezoni mwa miji na vijijini katika umbali usiozidi mita mia nne (400) na vile vile, kudhibiti upotevu wa maji ili huduma hii muhimu iweze kuwafikia wananchi wengi zaidi. Sera inatambua vile vile, kwamba Maji ni raslimali muhimu, adimu sehemu nyingi, huduma zake ni gharama, na uendelevu wake unahitaji utunzaji wa mazingira. Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mamlaka za Maji Mijini ni mkutano muhimu kwangu. Unanipa fursa ya kutoa tathmini ya kitaifa ya hali ya maji mijini.

**2. Umuhimu wa Sekta ya Maji:**

**Ndugu Wajumbe,** mikutano hii ya mwaka ya Mamlaka za Maji ni muhimu. Lakini mkutano huu ni muhimu zaidi, hasa tukizingatia kwamba huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani unaotarajiwa kufanyika rasmi mwezi Oktoba. Kwetu sisi wahusika tunaambiwa presha inapanda na inashuka. Ukweli ni kwamba kuanzia sasa mpaka Oktoba presha itakuwa inapanda tu, tunachopishana ni kasi ya kupanda.

**Ndugu Wajumbe,** kwa kutambua hali isiyoridhisha ya huduma ya maji safi mijini na vijijini, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 ibara ya 67 (a) imetoa mwongozo na lengo katika kutekeleza majukumu yetu ambayo yameainishwa katika Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 kwa kufanya yafuatayo, nanukuu:

***"Kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kupata maji safi, salama na ya kutosha kwa matumizi yao..... na kuwafikishia huduma hiyo asilimia 90 ya wakazi wa mijini na asilimia 65 ya wakazi wa vijijini ifikapo mwaka 2010",*** mwisho wa kunukuu.

Ibara hii inatilia umuhimu wa kuwapatia wananchi majisafi, salama na ya kutosha kwa matumizi ya kila siku karibu na makazi yao. Napenda kurudia tena maneno ya hekima aliyoyatoa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake ya kufungua Bunge la Tanzania tarehe 30 Desemba, mwaka 2005, nanukuu;

***"Tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania mijini na vijijini. Ndiyo kero nambari wani. ..... Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia kulikabili tatizo hili ..... Itaweka msukumo mpya katika kuwawezesha wananchi wengi zaidi mijini na vijijini kupata maji salama"*** Mwisho wa kunukuu.

Maneno niliyoyanukuu ni mazito, na changamoto muhimu kwetu katika kuongeza juhudi na kuhakikisha kwamba kusudio la Serikali la kukabiliana na tatizo la maji linatekelezwa ipasavyo.

**Ndugu Wajumbe**, upatikanaji wa maji safi na ya kutosha ni kichocheo muhimu cha kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Hivyo, ni dhahiri kwamba kuwepo kwa maji ya kutosha kwa matumizi mbalimbali na hasa mchango wake mkubwa katika mkakati wetu wa kuondoa umaskini ifikapo 2025 ni muhimu sana. Kwa kujua hilo, Wizara imezingatia Sera yake ya maji ya mwaka 2002, Ilani ya Uchaguzi na Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) katika kuandaa mipango na kuweka mwelekeo mpya ambao ulilenga kuziwezesha Mamlaka za Majisafi na Majitaka mijini kuwapatia maji safi wakazi wa miji ya makao makuu ya Mikoa kutoka asilimia 76 mwaka 2005 hadi asilimia 90, na huduma ya majitaka kutoka asilimia 16 kufikia asilimia 30, ifikapo mwaka 2010. Kwa upande wa maeneo ya vijijini, lengo lilikuwa kuwapatia wananchi maji safi na salama kutoka asilimia 55.7 mwaka 2005 hadi asilimia 65 ifikapo mwaka 2010. Kama dira ya maendeleo inavyoelekeza, huduma hii inabidi ifike asilimia 100 ifikapo mwaka 2025.

Kwa kuzingatia mikakati tuliyojiwekea, na kwa mujibu wa malengo ya MKUKUTA, bado tupo nyuma. Baadhi ya mapungufu yaliyojitokeza hususan, katika kufikia malengo ya MKUKUTA yamesababisha kufanyika mapitio ya malengo hayo na kuweka malengo mapya. Utekelezaji wake utazingatia vipaumbele kulingana na uwezo wa kifedha na utendaji katika kukamilisha miradi tuliyonayo kwa sasa na kufikia malengo hayo mapya. Sababu kuu zilizotufanya kupitia upya malengo ya awali ni kuchelewa kukamilika kwa miradi mingi kutokana na taratibu za manunuzi zilizochukua muda mrefu, hasa kwa miradi iliyohitaji idhini ya Benki ya Dunia, na uwezo wetu

mdogo katika kukabiliana na changamoto hii. Sisi tunazilaumu taratibu za manunuzi, lakini wasimamizi wa taratibu hizi wanatulaumu sisi kwa kutokuwa makini katika kuzizingatia.

Kutokana na umuhimu wa Sekta ya Maji kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na hifadhi ya mazingira katika kipindi cha muda wa kati kuanzia 2010/2011 hadi 2015/2016, Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa lengo la kuboresha usimamizi wa rasilimali za maji na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 58.7 hadi kufikia asilimia 65 mwaka 2015. Kwa upande wa huduma ya maji mijini, katika Miji Mikuu ya Mikoa 19 lengo litakuwa ni kuboresha upatikanaji wa maji kutoka kiwango cha sasa cha utoaji huduma cha asilimia 84 hadi kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2015. Jiji la Dar es Salaam, lina changamoto za kipekee. Zaidi ya asilimia 10 ya Watanzania wote hukaa katika Jiji hilo. Kasi ya ongezeko la watu la asilia, na kutokana na uhamiaji kutoka bara ni kubwa. Mipango ya Jiji imeelemewa na ongezeko hilo, kasi ya ongezeko la makazi ni kubwa kuliko mpango na huduma ya maji. Tumeitumia takwimu ya asilimia 68 kama ndio idadi ya wakaazi wa Dar es Salaam wanaopata maji. Takwimu haibadiliki. Ukweli ni kwamba kiwango cha sasa ni kati ya asilimia 50 na 60. Lengo letu liwe ni kuwapatia wakazi wa Dar es Salaam asilimia 70 kwa angalau saa 18 kwa siku ifikapo mwaka 2015. Huduma ya maji katika miji midogo na miradi ya kitaifa bado ni duni. Tuanze kuongeza upatikanaji huko kutoka asilimia 53 ya sasa hadi kufikia asilimia 57 mwaka 2015. Malengo haya ni ya uhakika zaidi, tutayaweza na tutayafikia bila matatizo.

## 3. Maji na Usafi wa Mazingira Mijini

**Ndugu Wajumbe,** maudhui ya mkutano wa mwaka jana uliofanyika Mjini Babati mwezi Aprili, 2009 yalikuwa ***"Maji na Mazingira".*** Maudhui haya yalitokana na ukweli kwamba huwezi kuzungumzia huduma endelevu ya maji mijini bila ya kugusia umuhimu wa kutunza mazingira. Mazingira yakiharibika maji hupotea na hivyo, kuathiri huduma nzima ya kuwapatia maji wananchi. Mengi yamefanyika katika kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi kwenye maeneo ya Mamlaka tangu mkutano huo wa mwaka jana. Nimefurahi kusikia kwamba maazimio ya Mkutano wa Babati kuhusu Mazingira pamoja na maazimio mengine yanayohusu kuboresha huduma, yameanza kutekelezwa kwa kasi nzuri. Hii ikiwa ni pamoja na Mamlaka kuanza kununua magari ya kusomba majitaka; kufanya ukaguzi wa mazingira (*environmental audit*); na kudhibiti utupaji holela wa majitaka. Wizara inaandaa Kanuni za kutekeleza Sheria ya Rasilimali za Maji, Sheria Na.11 ya mwaka 2009, kuhusu vibali vya maji na majitaka (*discharge and water permits*).

**Ndugu Wajumbe,** katika mkutano wa mwaka jana, maazimio mengine yaliyofikiwa yalilenga katika kuboresha utendaji katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuweka vigezo vinavyokubalika kutafsiri kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji mijini (*water coverage)*;

(ii) Mamlaka zote kuwa na takwimu sahihi za wateja;

(iii) Kuongeza wateja wanaopata huduma ya uondoaji majitaka;

(iv) Kutunza mazingira ya vyanzo vya maji kwa kushirikiana na wadau na taasisi husika;

(v) Kuanzisha utaratibu wa kuziwezesha Mamlaka za daraja A kupata mikopo ya mitaji ya kuwekeza kwenye miundombinu ya maji; na

(vi) Kuanzisha utaratibu wa kutathmini kwa mtindo wa kibiashara, utendaji wa Mamlaka za maji kwa lengo la kuzipandisha daraja Mamlaka za Maji za Wilaya na Miji midogo na Miradi ya Kitaifa iliyoonesha kuwa na uwezo wa kujiendesha kibiashara.

Nimefurahi kupata taarifa kwamba maazimio ya mkutano uliopita yametekelezwa kwa kiasi kikubwa. Utekelezaji huo umehusu pamoja na mambo mengine, yafuatayo:

(i) Wataalam kutoka Wizara, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA), Wakala wa Takwimu *(National Bureau of Statistics - NBS)* na Halmashauri (LGAs) walikaa pamoja na kukubaliana vigezo vya upatikanaji wa huduma ya maji. Viwango hivyo ndivyo vilivyokubalika katika mapitio ya MKUKUTA hadi kufikia mwaka 2015;

(ii) Mamlaka zote zinaendelea kufanya uhakiki wa wateja ili kuwa na idadi kamili;

(iii) Wateja wanaopata huduma ya uondoaji majitaka wameongezeka kutoka 29,870 mwezi Desemba, 2008 hadi 36,611 mwezi Desemba, 2009;

(iv) Kwa upande wa utunzaji wa mazingira, Wizara kwa kushirikia na Baraza la taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imetoa mafunzo yanayohusu tahadhari za mazingira kabla na baada ya ujenzi wa miradi ya majisafi na majitaka;

(v) Wizara imefanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka 21 za Wilaya na Miji midogo na Miradi 7 ya Kitaifa ambazo zitapandishwa daraja kulingana na uwezo wa kila moja kujiendesha kibiashara.

Kwa niaba ya Wizara yangu, nachukua nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bodi zote, Watendaji na Watumishi wa Mamlaka zote za Majisafi na Majitaka mijini kwa jitihada mnazozifanya kuhakikisha kwamba maazimio yaliyowekwa katika mkutano uliopita yanatekelezwa.

## 4. Masuala Muhimu na Changamoto za Utoaji wa Huduma

**Ndugu Wajumbe,** tofauti na miaka mingine, nimeambiwa kuwa katika mkutano wa mwaka huu majadiliano yatalenga kwenye kujadili masuala mbalimbali na changamoto zinazoendelea kutukabili katika Sekta ya maji. Pamoja na majadiliano hayo, mtapokea na kusikia mada mbalimbali za uzoefu kuhusu ukadiriaji wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi. Jambo hili limekuwa linaleta utata siku za hivi karibuni. Kwani hiki ni kiashiria muhimu sana katika kutekeleza malengo tuliyojiwekea. Katika mkutano huu mtapokea mada inayofafanua kwa kina namna ya kufikia ukadiriaji huo na mtapata mifano mizuri kutoka nchi nyingine namna bora ya kukadiria kiashiria hiki na mtazungumzia suala muhimu la jinsi ya kudhibiti upotevu wa maji *(Non Revenue Water (**NRW**))*.

Uvujaji wa maji mijini sasa ni asilimia 33 kwa Mamlaka 19 za Miji ya Mikoa na asilimia 53 kwa Jiji la Dar es Salaam. Hiki ni kiwango kikubwa cha upotevu wa maji ikilinganishwa na kiwango cha sasa cha kimataifa cha asilimia 20. Tuamue hapa kwamba ifikapo mwaka 2015 upotevu wa maji utadhibiwa na kufikia asilimia 30 kwa Mamlaka 19 za Miji mikuu ya Mikoa na asilimia 40 kwa Dar es Salaam. Lengo hilo litafikiwa kwa kuongeza ufungaji wa dira za maji, kukarabati mifumo ya maji iliyochakaa na kuhakiki uhalali wa wateja wanaopata huduma hiyo na kuwa na mfumo wenye ufanisi wa kuweza kufahamu na kurekebisha uvujaji wa maji. Katika suala hili tuwahusishe wananchi wa mijini katika kutoa taarifa za uvujaji ambao mara nyingi

haushughulikiwi, wananchi wakiona kwamba hili ni jukumu la Mamlaka za maji. Motisha itolewe kwa wanaojitolea kutoa taarifa. Gharama kwa Mamlaka itakuwa ndogo ikilinganishwa na upotevu mkubwa wa maji.

## 5. Ukaguzi wa Hesabu

Ukaguzi wa hesabu zetu na ripoti zake ni kioo cha kujipima utendaji wetu. Taarifa za ukaguzi wa hesabu kwa mwaka 2008/2009 zinaonyesha kuwa kwa Mamlaka za **Arusha**, **Kigoma**, **DAWASA** na **DAWASCO** hesabu zake zina walakini. Kwani wamepata vyeti vyenye mashaka *(Qalified)* ambapo, ukaguzi kwa Mamlaka nne (4) za **Musoma, Sumbawanga, Tabora na Singida** bado haujakamilika. Mwenendo huu haukubaliki hata kidogo. Hivyo, inabidi Wenyeviti wa Bodi pamoja na watendaji kuongeza nguvu katika usimamizi wa Mamlaka zenu na kuhakikisha hesabu za Mamlaka zinatayarishwa kwa usahihi unaokubalika, wenye viwango vya kimataifa *(International Financial Reporting System – IFRS)* na pia ukaguzi unafanyika kwa wakati kulingana na taratibu zilizopo.

**Ndugu Wajumbe**. Baada ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC) kupitia Hesabu za Mamlaka za maji Mijini za mwaka 2007/2008 matatizo yafuatayo yaliainishwa:

(i) Baadhi ya wakaguzi walionekana kuwa hawana utaalam wa kutosha au hawafuati maadili ya kazi zao (*lack of competency and non-adherence to professional ethics*) hivyo, kuandaa taarifa za ukaguzi zilizo chini ya kiwango cha ubora kinachotakiwa.

*(ii)* Hesabu kutayarishwa bila kufuata viwango vya *IFRS.*

(iii) Kutozingatiwa kwa bajeti kwa lengo la kubana matumizi.

(iv) Baadhi ya Mamlaka hazijaanzisha vitengo vya manunuzi na ukaguzi wa ndani.

(v) Baadhi ya Mamlaka bado wanadai madeni makubwa kwenye taasisi mbalimbali kwa mfano, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), usalama, shule na hospitali.

Mamlaka ambazo hesabu zao zilikuwa na matatizo ni pamoja na Kigoma, Mbeya, Singida, Shinyanga, Dodoma, Bukoba na Lindi. Nachukua nafasi hii kutoa maelekezo yafuatayo:

(i) Mawasiliano yafanywe kati ya Wizara na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ili kuhakikisha kuwa wanapelekwa wakaguzi wenye sifa stahili za kufanya ukaguzi kwa usahihi hivyo kuzisaidia Mamlaka kujua udhaifu wao na kujirekebisha.

(ii) Wizara ishirikiane na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuandaa mafunzo kwa wahasibu haraka iwezekanavyo.

(iii) Mamlaka ambazo hazina vitengo vya manunuzi na ukaguzi wa ndani *(Procurement and internal Audi Unit)* ziwe zimeanzisha vitengo hivyo ifikapo Desemba 2010.

(iv) Hesabu zitayarishwe kwa kufuata mfumo wa IFRS na bajeti zizingatiwe.

(v) Kwa upande wa madeni ya taasisi za umma kwa Mamlaka namwagiza Mkurugenzi wa Maji kibiashara amshauri Katibu Mkuu njia bora ya kufuatilia suala hili.

Ni matarajio yangu kwamba, matatizo yaliyoainishwa hayatajitokeza katika Hesabu za mwaka wa fedha 2008/2009.

## 6. Tathmini ya Utendaji

**Ndugu Wajumbe,** tathmini ya mwaka 2008/2009 na Julai 2009 hadi Desemba 2009 inaonyesha kuwa kwa viashiria vingi, hali ya huduma ya maji ni bora zaidi ikilinganishwa na mwaka 2007/2008. Hali ya uzalishaji maji katika Mamlaka za miji mikuu **19** ya mikoa imeongezeka hadi kufikia mita za ujazo milioni **110** ikilinganishwa na mita za ujazo milioni **104** mwaka 2007/2008, sawa na ongezeko la asilimia **6**. Ufungaji wa dira za maji umeongezeka hadi kufikia dira **217,110** ilipofika mwezi wa Desemba 2009, sawa na asilimia **89** ya wateja wote kwenye miji ya makao makuu ya mikoa. Lengo lilikuwa kuwafungia dira za maji wateja wote (100%) wa maji mijini ifikapo mwaka 2010. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, hadi kufikia mwezi Desemba, 2009 DAWASCO ilikuwa na jumla ya wateja hai **83,374** kati yao, asilimia **74.3** wamefungiwa dira za maji.

Ukusanyaji wa maduhuli umeongezeka kutoka shilingi bilioni **28.79** mwaka 2007/2008 hadi kufikia shilingi bilioni **34.88** mwaka 2008/2009. Pamoja na ongezeko hilo, mfumuko wa bei wa mwaka 2008/2009 ukizingatiwa, ongezeko halisi kwa maana ya uwezo wa kifedha wa Mamlaka ni dogo, na pengine limepungua. Uwezo wa manunuzi umeshuka.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Desemba 2009, Mamlaka zimeweza kukusanya kiasi cha shilingi bilioni **18.5** kutoka kwa wateja wanaotumia huduma ya maji ikilinganishwa na shilingi bilioni **15.9** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2008. Tahadhari niliyoitoa kuhusu ongezeko halisi inahusu ongezeko hilo. Idadi ya vioski imeongezeka kutoka **1,674** mwezi Juni, 2009 hadi kufikia **1,964** ilipofika mwezi wa Desemba 2009. Kwa upande wa DAWASCO, ukusanyaji wa maduhuli ulipanda kutoka shilingi bilioni **20.91** hadi kufikia Shilingi bilioni **22.12.** Katika kipindi cha Julai-Desemba, 2009 imeweza kukusanya kiasi cha shilingi bilioni **13.48** kutoka kwa wateja wanaotumia huduma ya maji ikilinganishwa na Shilingi bilioni **10.16** zilizokusanywa katika kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka 2008. Narudia tena kwamba tusishawishike kufurahia takwimu hizi kwani ongezeko halisi ni dogo au hasi. Pamoja na yote haya, nafurahi kusikia kwamba, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2009, DAWASCO imeweza kulipa pango la kiasi cha shilingi milioni **100** kwa DAWASA kila mwezi.

Kukamilika kwa mradi wa Kahama/Shinyanga kumeboresha huduma ya maji katika miji ya Shinyanga na Kahama. Huduma hiyo imeongezeka kutoka asilimia **60** hadi kufikia asilimia **91** mji wa Shinyanga na Kahama kutoka asilimia **40** hadi asilimia **70** na Mradi wa maji wa Jiji la Mwanza kutoka asilimia **84** hadi kufikia asilimia **90**. Changamoto inayotukabili ni kufikisha maji kwenye miji ya Tabora, Igunga na Nzega kutoka mradi wa Ziwa Victoria wa Kahama Shinyanga ifikapo mwaka 2015. Kukamilika kwa miradi hii, Mamlaka za Majisafi na Majitaka katika miji mikuu ya mikoa imeongeza idadi ya wateja katika kipindi cha mwaka 2008/2009 hadi kufikia **232,662** ikilinganishwa na wateja **214,667** wa mwaka 2007/2008, sawa na ongezeko la asilimia **8**.

**Ndugu Wajumbe,** mipango ya Mamlaka katika utunzaji wa takwimu na uandaaji wa ankara za maji kwa kutumia teknolojia ya kisasa ikiwa ni pamoja na kompyuta itaongeza tija na mapato. Ufungaji wa dira za maji utasaidia pia kuongeza mapato. Mwamko wa wananchi katika kulipia huduma wanazopata unazidi kuongezeka. Ubora wa maji yanayosambazwa kwa wateja umeongezeka katika baadhi ya maeneo kutokana na kutunza na kudhibiti vyanzo vya maji, kuboreshwa kwa mitambo ya kusafisha na kutibu maji, na kuongezeka kwa uwezo wa Mamlaka

kugharamia ununuzi wa madawa ya kutibu na kusafisha maji. Katika kuboresha utoaji wa huduma, Mamlaka za maji mijini inabidi ziendelee kufunga dira za maji kwa wateja wake ili kudhibiti matumizi ya maji, kupunguza malalamiko ya wateja na kuongeza mapato. Katika malengo yaliyowekwa ilitarajiwa kuwa ifikapo 2010, wateja wote waliounganishwa kwenye mitandao wangekuwa wamefungiwa dira za maji kwa aslimia 100. Lengo hili halikufikiwa. Tuamue katika mkutano huu kwamba ifikapo mwaka 2012, wateja wote wa Mamlaka wawe wamefungiwa dira za maji.

**7. Mamlaka ngazi za Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa**

**Ndugu Wajumbe**, kutokana na mabadiliko ya Muundo wa Wizara Mwaka 2007 Mamlaka za Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo (107) na Miradi ya Kitaifa (6) ilikabidhiwa rasmi Wizarani na kuwekwa chini ya uratibu wa Idara ya Maji Kibiashara ikiwa katika kundi la daraja C. Mwaka 2007/2008 tathmini (*rapid assessment*) ilifanyika katika miji yote ili kuona hali halisi ya huduma katika miji hiyo. Mkutano mkuu wa Mamlaka wa mwaka 2009 uliofanyika mjini Babati ulishauri kwamba miji 21, pamoja na miradi 7 ya kitaifa ambayo ilionyesha ufanisi mzuri ifanyiwe tathmini ya kina ikijumuisha masuala ya kifedha, kiufundi, watumishi na taarifa nyinginezo na kuona namna ya kuweza kuzipandisha daraja ili ziweze kujiendesha kibiashara.

Katika kutekeleza ushauri huo, Wizara yangu imefanya tathmini kwa Mamlaka hizo 21 pamoja na Miradi 7 ya kitaifa kwa kuzingatia vigezo vya kujiendesha kibiashara. Vigezo vilivyotumika ni kama ifuatavyo;

(i) Uwiano wa uzalishaji wa maji na mahitaji ya maji kwa wananchi;

(ii) Kiwango cha upotevu wa maji;

(iii) Uwiano wa mapato na matumizi;

(iv) Gharama za nishati ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha Maji;

(v) Gharama za watumishi;

(vi) Taarifa za ukaguzi wa hesabu;

(vii) Uwezo na ujuzi wa wataalam waliopo;

(viii) Saa za upatikanaji wa huduma ya maji na idadi ya wakazi wanaopata huduma hiyo.

Kufuatia vigezo vya tathmini hiyo, Mamlaka za miji mikuu ya Wilaya na miji midogo ya Kondoa, Makambako, Ngara, Kahama, Liwale, Kyela, Itumba-Ileje, Tukuyu, Nzega na Pangani pamoja na miradi ya kitaifa ya Wanging'ombe, Chalinze na KASHWASA zinapanda kutoka daraja C na kuingia daraja B. Kuwa katika Daraja B ina maana kuwa Mamlaka hizi zimeonekana zina uwezo wa kulipia gharama zote za uendeshaji na matengenezo pamoja na watumishi kutokana na makusanyo yao ya maduhuli. Taratibu za kisheria zitafanyika haraka iwezekanavyo ili Mamlaka hizo ziweze kutangazwa kupanda daraja ifikapo Julai 1, 2010. Hii itakwenda sambamba na kuwekeana saini mikataba ya makubaliano *(MoU)* kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini *(performance monitoring) y*a karibu zaidi. Wizara yangu itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka

hizi ili katika kipindi cha mkataba wa miaka mitatu (3) ziweze kuingia daraja A. Kwa niaba ya Wizara yangu, nachukua fursa hii kuwapongeza Wenyeviti na Menejimenti husika kwa kazi nzuri waliyoifanya hadi kufikia hatua hiyo.

Kwa Mamlaka za miji ya Mpwapwa, Njombe, Same, Kibondo, Kasumulu, Mbalizi, Masasi, Mbinga, Namtumbo na Korogwe pamoja na miradi ya kitaifa ya Mugango-Kiabakari, Makonde, Maswa na *Handeni Trunk Main (HTM)***,** kutokana na kutofikia vigezo zitaendelea kuwa Mamlaka za Maji za daraja C.

**Ndugu Wajumbe,** pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Mamlaka katika kukusanya maduhuli, baadhi ya wateja wameendelea kuwa kikwazo kikubwa kwani hawalipii kwa wakati huduma wanazopata. Hali hii husababisha madeni ya wateja kuongezeka na kukwamisha utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa Mamlaka. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2009 jumla ya shilingi bilioni **7.62** zilikuwa zinadaiwa na Mamlaka ambapo kati ya hizo, shilingi bilioni **1.9** ni madeni ya asasi za serikali. DAWASCO inadai jumla ya shilingi bilioni **31.5** ambapo Asasi za Serikali zinadaiwa jumla ya shilingi bilioni **1.2.** Takwimu hizi zinaonesha kwamba tatizo kubwa si Serikali na taasisi zake, bali ni ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wateja binafsi. Hata hivyo, hii haina maana ya kupunguza umuhimu wa jukumu la kulipa kwa taasisi za Serikali.

**Ndugu Wajumbe,** pamoja na changamoto nyingi, Bodi zote zimejitahidi kutekeleza majukumu kwa kiwango cha zaidi ya asilimia 61. Mafanikio haya yametokana na uongozi na utekelezaji mzuri wa majukumu yenu. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza na kuwataka muongeze juhudi zaidi katika kuendeleza kwa kiwango cha juu majukumu yaliyo mbele yenu ili kuhakikisha kwamba malengo yaliowekwa yanafikiwa kwa ufanisi na kwa wakati uliopangwa.

## 8. Utekelezaji wa Programu ya Sekta ya Maji

**Ndugu Wajumbe,** kama nilivyokwisha kueleza hapo awali**,** malengo katika utekelezaji wa Programu ya Sekta ya Maji ni pamoja na kuziwezesha Mamlaka kufikia viwango vya Milenia katika utoaji huduma ya maji safi na uondoaji majitaka mijini. Malengo hayo yatafikiwa iwapo Mamlaka hizi zitajengewa uwezo wa kutekeleza majukumu yake. Ni dhahiri kwamba majukumu hayo yanategemea upatikanaji wa fedha na uwezo wa kiutendaji. Katika utekelezaji wa Programu pamoja na uwekezaji katika miundombinu, Mamlaka pia zinajengewa uwezo kiutendaji .

Katika utekelezaji wa Programu tangu ulipoanza mwaka 2007 hadi sasa mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Vifaa mbalimbali kama vile dira za maji, magari, pikipiki na kompyuta vimenunuliwa kwa ajili ya Mamlaka za maji za miji ya Bukoba, Babati, Lindi, Mtwara, Musoma, Iringa, Songea, Shinyanga, Singida na Sumbawanga.

(ii) Mamlaka ya Kigoma inaendelea kukamilisha taratibu za manunuzi;

(iii) Magari kwa ajili ya miji ya Wilaya, pikipiki kwa ajili ya miji midogo na ya wilaya 100 pamoja na miradi ya kitaifa.

(iv) Kompyuta kwa ajili ya Mamlaka za mikoa (11) zimesahauliwa.

(v) Zimenunuliwa Mita kubwa *(bulk meters)* na mita za kuwafungia wateja.

(vi) Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Dodoma imepatiwa vifaa vya kusafishia mfumo wa majitaka (*sewer cleaning tool and cess pit emptier truck*)

(vii) Wahandisi Washauri kwa ajili ya kufanya usanifu na kuandaa vitabu vya zabuni waliajiriwa na kuanza kazi katika miji 10 ya Moshi, Kigoma, Arusha, Shinyanga, Morogoro, Bukoba, Musoma, Tanga, Tabora, Dodoma na katika miji midogo kumi na nane (18),

(viii) Wahandisi Washauri wameajiriwa na wanaendelea na kazi za kusimamia ujenzi katika miji ya Babati, Lindi, Mtwara, Sumbawanga, Singida, Mwanza, Mbeya, Iringa na mradi wa Kitaifa wa Chalinze.

(ix) Mikataba kwa ajili ya uchunguzi katika miji ya mikoa na miji midogo kwa mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma na Mwanza inatarajiwa kusainiwa kabla ya mwezi Juni 2010.

(x) Taratibu za kupata Wahandisi Washauri kwa miji midogo iliyobaki zimeanza na zoezi hili linatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha ujao.

Kwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji miradi mingi imejengwa na kukamilika, na mingine iko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Miradi iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

(i) Mradi wa Maji wa Kahama – Shinyanga uliobuniwa na ujenzi wake kusimamiwa na Serikali umekamilika na kuzinduliwa tarehe 30 Mei 2009 na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Katika kipindi cha kati ya mwezi Januari 2009 na Desemba 2009, DAWASA iliendelea kutekeleza Mpango wa ukarabati na upanuzi wa Miundombinu ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (*Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Project DWSSP)* na maeneo ya Bagamoyo na Kibaha. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2010. Mpango huu unatekelezwa na Serikali kupitia DAWASA kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Raslimali ya Ulaya (EIB) kwa gharama ya Dola za Kimarekani Milioni **164.6**.

(iii) Ili kuongeza wingi wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, Serikali inatarajia kujenga bwawa la Kidunda ambalo litaongeza uhakika wa maji katika mto Ruvu, kuchimba visima virefu maeneo ya Kimbiji na Mpera, kupanua mitambo ya Ruvu Chini na Ruvu Juu na kujenga bomba la kufikisha maji Jijini.

(iv) Ujenzi na ukarabati wa miradi ya majisafi inayotarajiwa kukamilika hivi karibuni ni miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa ya Mbeya, Iringa, Singida, Babati, Lindi, Mtwara, Sumbawanga, na miradi ya majitaka katika miji ya Mwanza na Mbeya.

(v) Miradi ya kati na midogo ya majisafi ya ujenzi/ukarabati ambayo imekamilika na mingine itakamilika hivi karibuni ni ya miji midogo ya Utete, Mpwapwa, Ikwiriri, Kibiti, Igunga, Missungi, Mugumu, Mwanhunzi, Bariadi, Bunda, Mlowo na Vwawa. Vilevile, ukarabati na upanuzi wa mifumo ya maji ulifanywa kwa miji midogo zaidi ya 82 na Miradi yote ya kitaifa.

Fedha zilizotumika katika utekelezaji wa kazi hizo ni Dola za kimarekani milioni **250** kati ya Dola za Kimarekani milioni 480 zilizotengwa kwa kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji.

**9. Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu**

**Ndugu Wajumbe,** tathmini (*Mid Term Review*) ya utekelezaji wa Programu imefanyika ili kupata hali halisi ya mwelekeo. Tathmini hiyo imebaini mambo yafuatayo:

(i) Kuwepo kwa kasi ndogo katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

(ii) Utekelezaji kutofuata vipaumbele kutokana na uhaba wa fedha, na

(iii) Upungufu wa wataalam wanaoweza kusimamia kwa makini utekelezaji wa programu katika maeneo ya utekelezaji hususan, katika ngazi za mikoa na wilaya, na miradi ya Kitaifa.

Maeneo yenye upungufu ni pamoja na usimamizi wa fedha za miradi, manunuzi, utoaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi na ukusanyaji, uchambuaji na utunzaji wa takwimu.

Hali hii imeonyesha umuhimu mkubwa wa kulishughulikia ipasavyo eneo la kujenga uwezo (*Capacity Development)* kwa watendaji katika ngazi zote za Mamlaka za mikoa, Wilaya, Miji midogo na Miradi ya kitaifa. Ili kufanikisha eneo hili la kujenga uwezo, Wizara iliandaa mwongozo *Capacity Development framework* kwa ajili ya watumishi wa Sekta ya Maji ambapo watumishi wa Mamlaka walipatiwa mafunzo ya jinsi ya kuandaa mpango wa kujenga uwezo (*Capacity Development Plans (CD-Plan)* ili mipango ya kuzijengea uwezo itokane na uhitaji wa Mamlaka husika. Mamlaka 16 kati ya 20 ziko katika hatua mbalimbali za kukamilisha *CD-Plans* zao zitakazoanza kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2010. Mipango hiyo itahusu, mafunzo, kuboresha mazingira ya kazi na ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi.

Mipango iliyopo kwa sasa ni kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi hasa katika Mamlaka za Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa hususan katika fani ya uongozi, biashara (na huduma kwa wateja), sheria ya manunuzi, sheria ya maji, sheria ya kazi, kuandaa na kutoa ankara Mwelekeo wa utekelezaji ni wa kuzingatia vipaumbele katika mpango uliowekwa na kwa fedha zilizokadiriwa *(procurement plan)* ya kuweza kukidhi malengo yaliyowekwa ili kufikia viwango vya utoaji huduma kwa kipindi husika.

**Ndugu Wajumbe,** kama nilivyoeleza hapo awali kuwa, eneo la muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa programu hii ni kujenga uwezo katika ngazi zote za utendaji. Mwongozo katika zoezi zima la kuzijengea uwezo Mamlaka zote upo na ni wajibu wa kila Mamlaka kuandaa mpango utakaowezesha kuongeza uwezo wa utendaji. Ni matarajio yangu kuwa katika Mkutano wa mwaka ujao tutakuwa na taarifa nzuri ya utekelezaji katika eneo hilo bila kuacha yale ambayo tumeyawekea kipaumbele kwa wakati husika. Itakuwa vema kama kaulimbiu ya mkutano wa mwaka 2011 itakuwa **"Kuzijengea uwezo Mamlaka wa Rasilimali watu katika kutoa huduma endelevu".**

**10. Sheria Mpya ya Maji**

**Ndugu Wajumbe,** utekelezaji wa Sera ya Maji ya mwaka 2002 umepewa nguvu ya kisheria kulingana na *Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji*, na *Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira*, ambazo zilipitishwa na Bunge la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili, 2009. Mheshimiwa Rais ameweka saini Sheria hizo tarehe 12 Mei, 2009 na Waziri mwenye dhamana ya maji ametangaza tarehe 1 Agosti, 2009 iwe siku rasmi ya kutumika sheria hizo. Sheria hizo zimetangazwa katika Gazeti la Serikali *(GN Na 21* na *22)* za tarehe 22 Januari, 2010. Kwa mujibu wa Sheria hizo ya maji na usafi wa mazingira, maeneo muhimu ambayo ni mapya au yamefanyiwa mabadiliko hususan, uendeshaji shughuli za Mamlaka ni kama ifufuatavyo:-

(i) Tofauti na sheria iliyopita Waziri mwenye dhamana na Sekta ya Maji kwa kushirikiana na Waziri wa TAMISEMI sasa anauwezo wa kuziunganisha Mamlaka (*clustering)* ili kuzipa nguvu zaidi kujiendesha kibiashara. Kanuni *(Regulations)* zitakazotumika katika kuunganisha Mamlaka ziko katika hatua za mwisho kukamilishwa. Ili kuleta ufanisi zaidi, eneo la Mamlaka linaweza kwenda nje ya mipaka ya Halmashauri/Mji husika.

(ii) Wajumbe wa Bodi wataendelea kuwa kumi kwa Mamlaka za ngazi ya Mkoa na watateuliwa na Waziri Mwenye dhamana ya Maji kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI. Vile vile, Bodi za Wilaya na Miji Midogo zitakuwa na wajumbe wasiozidi saba na watateuliwa na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI. Mwongozo wa namna ya kuwapata wajumbe hawa umetumwa kwa wahusika. Maana yake ni kwamba usimamizi wa Mamlaka za maji katika miji ya wilaya na miji midogo unahamishiwa Serikali za mitaa kwenye halmashauri husika.

(iii) Ili kuharakisha uwekezaji kwenye Mamlaka, utaanzishwa mfuko wa Taifa wa Maji (*National Water Investment Fund*). Taratibu za namna ya kuanzisha na kuendesha mfuko huu zinaandaliwa.

**Ndugu Wajumbe**, nitumie fursa hii kuwakumbusha majukumu yenu ambayo yameainishwa katika Sheria Na. 12 ya mwaka 2009, kifungu Na. 20, kama ifuatavyo:

(i) Kutoa huduma ya maji kulingana na mahitaji na matumizi kwa kuhakikisha kuwa utunzaji na ubora wa maji unakuwa kwenye viwango vinavyotakiwa kwa kuzingatia mazingira;

(ii) Kuhakikisha kuwa huduma ya maji inakuwa endelevu na kufuatilia ubora wa maji kwa muda wote;

(iii) Kujenga na kutunza miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira;

(iv) Kutunza na kulinda vyanzo vya maji;

(v) Kuishauri Serikali katika utungaji wa Sera na miongozo inayohusiana na maji;

(vi) Kupanga na kutekeleza miradi mipya ya maji safi na usafi wa mazingira;

(vii) Kutoa elimu na taarifa mbalimbali kwa umma juu ya afya inayohusiana na maji, usafi wa mazingira pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo;

(viii) Kushirikiana na Halmashauri katika kuandaa mipango ihusuyo mambo ya maji na usafi wa mazingira;

(ix) Kukusanya maduhuli na ushuru unaohusiana na utoaji wa huduma mbalimbali;

(x) Kutoa mapendekezo ya bei mpya za maji; na

(xi) Kuingia mikataba mbalimbali kwa kupitishwa na Bodi za Mamlaka itakayokuwa na manufaa kwa Mamlaka.

Madhumuni haya yapo bayana na naomba myazingatie.

## 11. Kuunganisha Mamlaka za Maji (*Clustering of Water Utilities*)

Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha huduma za maji katika miji midogo na miradi ya kitaifa, eneo ambalo lina upungufu mkubwa wa wataalam wa kusimamia uendeshaji wa Mamlaka. Kwa kuzingatia hali ya Mamlaka katika miji midogo, Mamlaka za miji mikuu ya mikoa imezisaidia Mamlaka ndogo kama ifuatavyo:

(i) Mamlaka za miji ya mikoa zimesimamia ujenzi wa miradi mikubwa na midogo katika miji midogo. Kwa mfano, Mamlaka ya Mbeya imesimamia ujenzi wa mradi wa maji wa mji wa Mlowo, Mamlaka ya Mwanza imesimamia miradi ya miji ya Misungwi na sasa itasimamia mradi wa maji Lamadi, na Mamlaka ya Musoma imesimamia mradi wa maji mji wa Mugumu. Mamlaka ya Moshi inasimamia uborishaji wa huduma Mwanga.

(ii) Miji midogo imeunganishwa na miji ya mikoa katika kazi za kishauri (*consultancy services*). Hivyo, Mamlaka za miji mikuu ya Mikoa ndizo zinazoingia mikataba na kampuni za ushauri ambapo kazi za usanifu, uandaaji wa vitabu vya zabuni na usimamizi wa ujenzi zinaendelea kwa baadhi ya mji hapa nchini.

(iii) Tumezitumia Mamlaka za miji mikuu ya mikoa katika tathimini za haraka za hali ya maji vijijini. Tanga imetusaidia Lushoto, Mtwara imetusaidia Lulindi, Tabora imetusaidia Urambo.

(iv) Mamlaka ya Mbeya imeingia mkataba, imelaza bomba na inaiuzia maji (bulk water) kwa Mamlaka ya mji mdogo wa Mbalizi.

Nichukue nafasi hii kuzipongeza Mamlaka za Mikoa ambazo kwa dhati kabisa zimebeba jukumu hili kubwa kwa lengo la kuwapatia Watanzania wenzetu maji safi na salama. Wizara yangu bado iko katika kuandaa utaratibu mzuri wa kuunganisha Mamlaka za Maji kwa njia ambayo itakubalika na pande zote husika na kuleta tija katika sekta ya maji. Katika suala hili inabidi tuwe makini na tusiende kwa pupa. Tuimarishe mafanikio tuliyoyapata mpaka sasa. Naamini washiriki wenzetu katika sekta watatuelewa.

## 12. Huduma kwa wateja

**Ndugu Wajumbe,** bado hatujafikia kiwango kinachotakiwa katika kutoa huduma kwa wateja mbali na ukosefu wa maji. Malalamiko tunayoyapata yanahusu ankara, kukatiwa huduma ya maji hata pale ambapo malipo yanafanyika, kutopatiwa majibu ya malalamiko yao, ni lugha isiyoridhisha ya watoa huduma. Nina mfano wa mteja ambaye amelalamika kuwa amefungiwa dira ya maji ya viwandani ingawa ni nyumba ya kawaida ya kuishi. Sekta ya Maji ni sekta hodhi au yenye ukiritimba, tuna wajibu wa kuhakikisha malalamiko ya wateja yanasikilizwa na wanajibiwa. Inatubidi tujitangaze zaidi hasa kuhusu wajibu wa EWURA na Baraza la watumiaji

wa huduma za EWURA katika kuongeza ufanisi wa Mamlaka zetu katika kumhudumia mteja. Pamoja na ukiritimba wa Sekta ya Maji, kama maji ni biashara, basi bado “mteja ni mfalme”.

## 13. Miradi inayoendelea

**Ndugu Wajumbe,** baadhi ya miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na;

i. Mradi wa maji wa Masasi Nachingwea ambao utagharimiwa chini ya program ya maji. Zabuni itafunguliwa tarehe 29 Aprili 2010 na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Julai 2010. Ujenzi wa miradi ya maji katika miji ya Orkesment, Kateshi na Karatu pia unatarajia kuanza mwaka ujao wa fedha.

ii. Mradi wa Same-Mwanga-Korogwe utagharimu kiasi cha USD 147 milioni. BADEA, OPEC Fund (OFID) na Serikali tutatoa kiasi cha USD 35.76 milioni kwa ajili ya kujenga chanzo, chujio na matanki ya kuhifadhi maji. Kwa awamu ya kwanza ufadhili huu utawezesha kuwapatia maji vijiji 8 (Same vijiji viwili na Mwanga vijiji 4) vilivyo karibu na chanzo. Ujenzi wa miradi ya maji katika miji ya Same na Mwanga unatarajiwa kutekeleza katika awamu ya pili fedha zitakapopatikana.

iii. Chini ya ufadhili wa *ACP-EU Water Facility* utafanyika upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa vitabu vya zabuni kwa miundombinu ya majisafi na majitaka itakayokidhi mahitaji hadi mwaka 2025 kwa miji ya Bukoba, Babati, Lindi, Kigoma, Mtwara, Musoma na Sumbawanga. Kazi hiyo itafanywa na M/s Poyry na mkataba utasainiwa mwezi huu April 2010 na kazi itaanza Mei 2010 na itafanywa kwa miezi 15 kwa gharama ya Euro 2.277 millioni.

Mradi wa maji katika mji wa Mugumu uko katika hatua za mwisho za ukamilishaji nsa utazinduliwa na Mhe Rais hivi karibuni. Nachukua nafasi hii kuipongeza sana Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Musoma kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kusimamia ujenzi wa mradi huu. Asanteni sana.

## 14. Mambo Muhimu ya kuzingatia

**Ndugu Wajumbe,** changamoto zilizopo ni nyingi na inabidi tuongeze nguvu ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa Mamlaka zenu ili kuongeza kasi ya ufanisi katika kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wanaoishi kwenye miji yenu. Dhamana mliyopewa na Serikali ya kuzisimamia Mamlaka hizi ni kubwa. Jambo muhimu ni kuhakikisha mnakuwa na matumizi stahiki kulingana na bajeti zenu. Hesabu safi (*Clean Certificate*), ni dalili nzuri na inaonyesha uhai wa Mamlaka mbele ya umma na wafadhili pia.

Napenda kuwaagiza mambo muhimu yafuatayo ili myazingatie katika utekelezaji wa majukumu yenu kwa madhumuni ya kufikia malengo tuliyojiwekea ya utoaji huduma ya maji na uondoaji wa majitaka kwa muda uliopangwa:-

(i) Bodi kusimamia Mamlaka ili ziendeshwe kwa uwazi, na kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria zilizopo.

(ii) Kuwaendeleza watumishi kwa kuwajengea uwezo na kuwapa motisha kulingana na taratibu zetu tulizojiwekea pamoja ili waweze kubaki na kuzitumikia Mamlaka kulingana na mikataba.

(iii) Mtatakiwa na kushauri jinsi gani mnaweza kutumia na tunaweza kuiboreshaTaasisi yetu ya Maendeleo ya Raslimali za Maji (Water Resources Development Institue).

(iv) Kuandaliwa kwa mipango ya wafanyakazi wa Mamlaka mbalimbali ya mafunzo kutembeleana (*exchange program*). Sio lazima mafunzo yote yafanyika nje ya nchi.

(iv)Uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi ufanyike kwa usahihi na kwa wakati.

(v) Kusimamia kwa karibu miradi inayoendelea kutekelezwa badala ya kuwaachia Wahandisi Washauri peke yao.

(vi) Kuwepo kwa uhusisano mzuri wateja na wadau wetu, taratibu zilizopo pamoja na sera za malipo (*credit policy*) zitumike ipasavyo na zifanyiwe mapitio ya mara kwa mara ili ziende na wakati.

**Ndugu Wajumbe,** mikataba mliyowekeana na Wizara yangu ndio mhimili wa kufikia malengo tuliyojiwekea. Napenda kuchukua fursa hii kusisitiza kuwa Mamlaka ziwasilishe taarifa zote zilizoainishwa kwenye Mikataba ya Makubaliano (MoU), *Performance Agreement* zikiwemo Taarifa za Utendaji, Hesabu na Ukaguzi wa ndani kila robo mwaka na mwaka kwa mfumo unaotakiwa na kwa wakati. Suala la Bodi kujitathmini utendaji wake na kumtathmini Mkurugenzi kulingana na vigezo, ama mikakati mliyoweka kwenye Mamlaka zenu ni jambo zuri na ni ndio utawala bora. Tathmini hii imewekwa kwa makusudi na misingi yake mikuu ni kumsaidia waziri mwenye dhamana na Sekta ya maji kufanya maamuzi ya haki.

Kupitia Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira, Mamlaka zimepewa uhuru (*autonomy*) mkubwa sana, kiasi kwamba kuna Bodi zinashindwa kuutumia uhuru huu vizuri kufanya maamuzi kwa wakati muafaka. Napenda kusisitiza kwamba mawasiliano ya kiutendaji ya taasisi za Wizara na zile zilizo nje ya Wizara hayana budi kufanyika kwa kufuata utaratibu na ngazi zinazokubalika.

Lengo kuu la Mkutano huu, pamoja na mambo mengine, ni kupata taarifa za hesabu zilizokaguliwa. Tofauti na miaka miwili iliyopita, mwaka huu Mamlaka zenye hati za mashaka *(Qualified)* zimeongezeka na Mamlaka 4 hesabu zao bado hazijakamilika. Mwenendo huu haukubaliki. Wenyeviti wanaohusika wanatakiwa wakihakikishie kikao hiki kwamba jambo hili halitajirudia katika mwaka ujao.

## 15. Shukrani

**Ndugu Wajumbe,** mafanikio haya tunayojivunia sasa yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na michango kutoka kwa nchi marafiki na taasisi zake. Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliohusika kwa njia moja ama nyingine kuleta mafanikio haya. Miongoni mwao ni Serikali ya Ujerumani kupita Mashirika ya Maendeleo ya GTZ na KfW, Shirika la Maendeleo la Denmark, Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Shirika la Maendeleo la Norway, Shirika la Maendeleo la Uswisi, Shirika la Maendeleo la Japan, Shirika la Ufundi la Ubelgiji, Shirika la Milenia la Marekani, Shirika la Makazi Duniani, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo ya Nchi zinazotoa mafuta (FAO) Benki ya Uwekezaji ya Nchi za Ulaya, pamoja na wadau wengine wengi ambao

wamekuwa wakichangia katika kuhakikisha Sekta ya Maji inakuwa endelevu. Nawashukuru sana na naomba waendelee na moyo huo.

## 16. Hitimisho

**Ndugu Wajumbe,** nawashukuru wote waliohusika katika maandalizi mazuri ya Mkutano na pia kwa usikivu wenu. Ninapohitimisha, napenda kurudia kusisitiza mambo yafuatayo**:**

(i) Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na kufikia malengo ya MKUKUTA, ya milenia, na Dira ya maendeleo 2025.

(ii) Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kupunguza uvujaji wa maji mijini, kila Mamlaka ijipangie mikakati ya kupunguza kwa kiwango kikubwa cha maji yanayovuja.

(iii) Wizara ishirikiane na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ili wapelekwe wakaguzi wenye sifa, na mafunzo kwa wahasibu yatolewe.

(iv) Mamlaka zianzishe vitengo vya manunuzi kabla ya Desemba 2010 kwa ambazo hazina, hesabu zitayarishwe kwa kufuata mfumo wa IFRS na bajeti zizingatiwe.

(v) Wizara izisaidie Mamlaka katika kufuatilia ulipwaji wa madeni.

Kwa mujibu wa Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, uendeshaji wa shughuli za Mamlaka utazingatia yafuatayo:

(i) Waziri mwenye dhamana na Sekta ya Maji kwa kushirikiana na Waziri wa TAMISEMI sasa anao uwezo wa kuziunganisha Mamlaka (*clustering*) ili kuzipa nguvu zaidi ya kujiendesha Kibiashara. Natarajia kuwa Kanuni (*Regulations*) zitakazotumika katika kuunganisha Mamlaka zitakamilishwa kabla ya Julai 2010.

(ii) Bodi za Wilaya na Miji Midogo zitakuwa na wajumbe wasiozidi saba na watateuliwa na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI.

(iii) Ili kuharakisha uwekezaji kwenye Mamlaka, utaanzishwa mfuko wa Taifa wa Maji (*National Water Investment Fund*).

Mambo mengine muhimu yanayohitaji kuzingatiwa ni pamoja na yafuatayo:

(i) Mamlaka za Maji mijini, EWURA na Baraza la Usuluhishi la EWURA Wizara na tuzingatie wajibu wetu wa kuhakikisha kero kwa wateja zinapungua

(ii) Bodi zisimamie Mamlaka ili ziendeshwe kwa uwazi, na kufuata taratibu, kanuni na sheria zilizopo.

(iii) Watumishi waendelezwe kwa kuwapa motisha kulingana na taratibu zilizopo

(iv) Kuandaliwe kwa mipango ya wafanyakazi wa Mamlaka mbalimbali kutembeleana (*exchange program*) kwa ajili ya mafunzo na kubadilishana uzoefu.

(v) Uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi zifanyike kwa usahihi na kwa wakati.

(vi) Mamlaka zisimamie kwa karibu miradi inayoendelea badala ya kuwaachia Wahandisi Washauri peke yao.

(vii) Kuwepo kwa uhusiano mzuri na wadau wetu, taratibu zilizopo pamoja na sera za malipo (credit policy) zitumike ipasavyo na zifanyiwe mapitio ya mara kwa mara ili ziende na wakati.

(viii) Nafasi ya Mdhibiti wa Sekta (EWURA) ni muhimu sana katika kuyafikia malengo yetu. Mamlaka zizingatie taarifa ya utendaji wenu atakayotoa.

Nazitakia kila la heri Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka za Maji nchini katika kuhakikisha tunawapatia wananchi huduma zilizo bora, zenye uhakika na endelevu kwa gharama nafuu. Kwa wale Wenyeviti ambao muda wao wa kuwa kwenye Bodi unakwisha mwaka huu, ninachukua fursa hii kuwashukuru sana kwa ushirikiano mlioonesha katika kipindi chote mlipokuwa kwenye Bodi hizi.

Nawashukuru tena wote mlioitikia wito wa kuja kushiriki katika mkutano huu muhimu ambao msukumo wake ni kujadili changamoto zinazozikabili Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini katika uendeshaji na utoaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka kwenye miji husika.

Nawashukuru wenyeji wetu wa Mara, Mhe. Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala na Viongozi wengine kwa kutukaribisha. Namshukuru mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Musoma pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wake kwa kazi kubwa ya maandalizi ya Mkutano.

Si kawaida kwa Waziri kuwashukuru watendaji wake kwani na yeye ni sehemu ya Wizara. Hata hivyo, Katibu Mkuu amefanya kazi kubwa kuhakikisha Mkutano unafanikiwa katika hili amesaidiwa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Maji Kibiashara (Maji Mijini) Ndugu Samuel Lupimo ambaye amestaafu jana tarehe 26 Aprili, 2010 na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maji Kibiashara Bi. Onike Dorcas Mrema. Mratibu wa maandalizi yote haya ni Bi. Elizabeth Kingu, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Maji Kibiashara.

Nachukua fursa hii kuwakaribisha Tukuyu kwenye Mkutano wa 13 wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka mjini utakaofanyika mwaka 2011. Baada ya kusema hayo, napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha tena kwenye Mkutano huu na kuwataka sasa tuanze kazi iliyotuleta hapa Musoma. Sasa, napenda kutamka kwamba Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini sasa umefunguliwa rasmi.

# MAJI NI UHAI NA USAFI WA MAZINGIRA NI UTU

**PROF. MARK J. MWANDOSYA (MB)**
**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**